Jacob Mushi



Siri 7 za Kuwa Hai Leo

- Msingi wa Maisha yenye Mafanikio -

SIRI 7 ZA KUWA HAI LEO

(Msingi wa Maisha yenye Mafanikio)

Hatimiliki © Mwandishi

JACOB MUSHI
TANZANIA.
EAST AFRICA.
Simu: +255 654 726 668
Barua pepe: jcobtz@gmail.com
Web: www.jacobmushi.com

Toleo la Kwanza – February, 2017

ISBN: **978-9976-5051-0-8**

Haki Zote Zimehifadhiwa.

Hakuna sehemu yoyote ya kitabu hiki ambayo inaruhusiwa kutolewa upya au kuhamishwa kwa namna au njia yoyote; kielektroniki au kiufundi au kwa kutoa nakala (photocopy), kurekodi kwa namna yoyote ya kuhifadhi habari au kurudishia tena bila ruhusa ya maandishi kutoka kwa mwandishi. Kwa matumizi ya kitabu hiki katika mafundisho tafadhali wasiliana na mwandishi kwa mawasiliano yaliyopo hapo juu.

YALIYOMO

UTANGULIZI ix

SIRI 1: KUANDIKA HISTORIA MPYA.....**Error! Bookmark not defined.**

(A) KUANDIKA HISTORIA.....**Error! Bookmark not defined.**

(B) UTAONDOKA PEKE YAKO.....**Error! Bookmark not defined.**

SIRI 2: KUMALIZIA KAZI.....**Error! Bookmark not defined.**

(A) ONDOKA UKIWA MTUPU ..**Error! Bookmark not defined.**

(B) WAKATI SAHIHI NI LEO.....**Error! Bookmark not defined.**

SIRI 3: KUTENGENEZA ULIPOHARIBU..**Error! Bookmark not defined.**

(A) HUWEZI KUFUTA MAKOSA YAKO ....**Error! Bookmark not defined.**

(B) JIFUNZE KUPITIA MAKOSA YAKO.....**Error! Bookmark not defined.**

SIRI 4: KULITIMIZA KUSUDI .....**Error! Bookmark not defined.**

(A) KUSUDI NI NINI? .....**Error! Bookmark not defined.**

B) KULIISHI KUSUDI .....**Error! Bookmark not defined.**

SIRI 5: KUVUMBUA.....**Error! Bookmark not defined.**

(A) UBUNIFU WA VITU VIPYA..**Error! Bookmark not defined.**

B) KUENDELEZA MAWAZO YA WENGINE .**Error! Bookmark not defined.**

SIRI 6: KUGUSA MAISHA YA WENGINE .....**Error! Bookmark not defined.**

(A) KUTOA ULICHONACHO KWENYE JAMII..**Error! Bookmark not defined.**

(B) ONGEZA THAMANI KWENYE MAISHA YA WENGINE**Error! Bookmark not defined.**

SIRI 7: KUSHINDA.....**Error! Bookmark not defined.**

(A) ULIZALIWA MSHINDI.....**Error! Bookmark not defined.**

(B) UFANYEJE UENDELEE KUSHINDA?...**Error! Bookmark not defined.**

SHUKRANI

Wapo watu wengi sana wamehusika katika kuniwezesha mimi kufikia hapa nilipo hadi kutoa kitabu hiki. Wapo niliowapa kipaumbele cha kuwepo kwenye kitabu hiki kwa maana nisingeweza kuwaandika wote.

Kwanza kabisa napenda kutoa shukrani zangu kwa Mungu mkuu muumba wa vyote na anaetupatia uwezo, akili na maarifa kwa ajili ya kuifanya dunia kua sehemu bora zaidi.

Mama yangu mzazi, Wesael Moshi, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa mama yangu mzazi alienilea katika maadili na nikaweza kufika hapa nilipo. Ametutunza na kutuonyesha njia bora ambazo tunazitumia ili kufanikiwa. Ametuvumilia pale tulipomkosea. Kitabu hiki kikawe furaha kwake kwa kutambua kua alizaa mtoto wa pekee sana duniani. Mungu akubariki na kukuongezea maisha marefu duniani ufaidi matunda ya watoto wako.

Kaka yangu, Daudi Mwakalinga, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako kwa kuwa kaka mzuri sana na mshauri wangu pale ninapokua kwenye wakati mgumu. Amekuwa akinihamasisha sana na kunionyesha umuhimu wa kusoma vitabu na mambo mengine mengi sana Mungu akubariki na kukipa maisha marefu Zaidi uendelee kufanyika Baraka kwa wengine.

Mchungaji wangu, Allen Lekey, namshukuru sana huyu mtu wa Mungu ambaye amefanyika Baraka katika familia yetu amekua kama baba kwetu ametusomesha na kutulelea kiroho ndio maana unayaona matunda haya katika kitabu hiki. Mungu akubariki sana na akuongezee maisha marefu na nguvu za kumtumikia uendelee kua Baraka kwa maisha ya wengi.

Kocha Wangu, Amani Makirita, Mwandishi wa Kitabu BIASHARA NDANI YA AJIRA, Amekua mshauri wangu wa biashara na ujasiriamali, amekua mtu ninaejifunza sana katika mafundisho yake na kunifanya na mimi kuchukua hatua ya kubadili maisha yangu Kupitia mitandao yake ya Kisima cha Maarifa na Amka Mtanzania. Mungu akuongezee maisha marefu yenye Baraka kwa wengi. Tupo wengi sana tunajifunza kwako.

Mwalimu wangu, Shemeji Melayeki, , Mwandishi wa Kitabu cha NGUZO ZA SIKU, amekua mtu wa pekee kwangu nilijifunza mambo mengi sana kwake nimeona kipawa chake cha Public Speaking na kikaamsha yale yaliyokua ndani yangu Pamoja na Harakati zake za kusoma vitabu zijulikanazo kama City Reading Champions (CRC). Mungu akuwezeshe utimize yale yote yaliyoko ndani yako.

Mwisho Kabisa ninapenda kuwataja watu wa muhimu pia kwangu ambao wamekuwa wakinishauri na kunipa nafasi mbalimbali za kufundisha katika vikundi ambavyo wameanzisha, Shukrani hizi ziwafikie Waandishi

wenzangu Lazaro Samwel mwandishi wa Kitabu cha NGUZO TATU ZA MAISHA na Joas Yunus Buyungu mwandishi wa kitabu cha INUKA. Watu hawa wamekuwa marafiki wazuri sana na tumeweza kufanya mambo makubwa kwa pamoja.

Nawashuru wote waliohusika kwa namna moja au nyingine kufanya hiki kitabu kukufikia.

MAONI YA WASOMAJI NA WAANDISHI WENZANGU.

"Kuwa Hai ni Zaidi ya kuwepo duniani, watu wengi sana wapo duniani lakini hawapo Hai, na wanaishi maisha ambayo si yao, Jacob Mushi kupitia Siri 7 za Kuwa Hai Leo ametengua kitendawili hicho, kwa kufichua mambo ya msingi ambayo ya kuishi maisha ya utoshelevu."

Street Pastor,

Masanja Mkandamizaji

"Huwezi kusoma kitabu hiki kisha ukabaki kama ulivyo. Uwe unafanya kazi au hufanyi kazi uwe mfanyabiashara, mjasiriamali au mwimbaji kama mimi, ukisoma Siri 7 za kuwa hai leo, ni lazima utaongezeka kwenda hatua nyingne."

Atosha Kissava

Mwimbaji wa Nyimbo za Injili Tanzania

"Yaani ukianza kukisoma hutamani kuacha kwa jinsi kimebeba 'facts' Watu wanaangamizwa kwa kukosa

maarifa kumbe yamo kwenye "SIRI 7 ZA KUWA HAI LEO." Ushauri wangu kwa Watanzania na wengine wanaoelewa kiswahili usikose nakala yako ya kitabu hiki kwenye library yako nyumbani. Thamani yake ni zaidi ya Tsh 10,000= utakayoitoa kukinunua. Hakika kitabadilisha maisha yako kuwa bora zaidi."

Regula Tarimo

Mjasiriamali.

"Siri 7 za kuwa Hai Leo, ni kitabu kinachotoa muongozo wa kuishi maisha ya kulitimiza kusudi lako kwa mafanikio na furaha, Jacob Mushi amewasilisha kwa lugha inayoeleweka siri saba zitakazokufanya ujitambue na uanze kuwa hai. Kwa mtu yeyote mwenye kutaka kuishi maisha ya ushindi leo na kuacha historia nzuri napendekeza asome kitabu hichi."

Mkurugenzi/CEO wa www.kilimo.net

Daudi Mwakalinga.

“Kitabu cha Siri 7 Za Kuwa Hai Leo ni kitabu ambacho kila mtanzania hapaswi kukosa kukisoma. Nimekisoma na nimeona nguvu iliyoko ndani ya kitabu hiki pia nimeshuhudia watu wengi wakitoa sifa tele za kuweza kubadili maisha yao kupitia kitabu hiki. Napenda kusema kitabu hiki ni kama lulu kwa kila mtanzania kuweza kujifunza na kubadili fikra na maisha yake. “

Lazaro Samwel

Kocha wa Maisha,mwandishi na Mjasiriamali.

Mtunzi na Mwandishi wa Kitabu cha NGUZO 3 ZA MAISHA

UTANGULIZI

SIRI 7 ZA KUA HAI LEO ni kitabu ambacho kinakufanya wewe ujitambue na utambue thamani ya uhai ulio nao leo. Unapotambua sababu za wewe kuwa hai leo huwezi kuchezea hata sekunde na utatumia nafasi hiyo vyema kutimiza siri hizi kila siku. Kitabu hiki kila mtu alie hai anapaswa kukisoma kwakua kimekwenda kumlenga kila mmoja kutokana na makusudi mbalimbali ambayo Mungu kayaweka ndani yetu.

Hukuzaliwa kwa bahati mbaya wala haupo hai kwa bahati mbaya. Wako wengi wa maana na wenye haki kuliko wewe wameshaondoka duniani wengine wakiwa hawajatimiza kile walichokijia duniani. Unafikiri wewe upo hai kwa bahati mbaya? Mtoto mdogo anazaliwa leo na anaondoka baada ya saa chache unadhani alikosewa kuzaliwa? Wewe haupo bure duniani ungeweza kwenda badala ya mtoto huyo aliyezaliwa na kufa papo hapo ili yeye aishi kama upo kwa bahati mbaya basi!

SIRI 7 ZA KUA HAI LEO zinakwenda kukufungua pale ulipofungwa na minyororo ya fikra na kukufanya ujitambue na kujiona una nafasi ya kipekee duniani. Haijalishi umefanya makosa ya aina gani, Haijalishi umezeeka kiasi gani bado kuwepo kwako hai ni kwa kusudi la Kimungu. Haijalishi umefikia mafanikio makubwa kiasi gani, bado kuna sababu ya wewe kuwepo hai leo.

Mungu haangalii umeanzaje anatazama unamalizaje hivyo wakati wa wewe kuwa makini sana ni wakati wako wa mwisho wakati wako ujao ndio wa muhimu kuliko wakati uliopita. Hata kama ulitenda mema kiasi gani yanaweza kupotezwa na kosa moja utakalolifanya kesho.

Jifunze siri hizi uzifanyie kazi na maisha yako yawe bora kwako na kwa wengine, uweze kulitimiza kusudi la Mungu ndani ya maisha yako.

Nikutakie kila la Kheri katika safari yako ya kutimiza kusudi lako. Ni Imani yangu utajifunza mengi sana ndani ya kitabu hiki na maisha yako hayakuwa kama yalivyokua.

Rafiki Yako,

Jacob Mushi